TANGAZO LA SERIKALI Na. 1044 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA ENEO LA MSITU WA SERIKALI ZA MITAA CHINYAMI YA MWAKA 2024

KWA KUWA, Eneo la Msitu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa Chinyami lilitangazwa kuwa Eneo la Msitu wa Serikali za Mitaa Chinyami chini ya Tangazo la Serikali Namba 442 la Mwaka 1989;

KWA KUWA, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kufanya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa Chinyami;

NA KWA KUWA, Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Sura ya 323 ambayo, pamoja na masharti mengine inamtaka, anapokusudia kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Serikali za Mitaa Chinyami ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Chinyami.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa Chinyami ni-

(a) kubadilisha hadhi kutoka msitu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa; na

(b) kuhifadhi baioanuwai, vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la Msitu wa Serikali za Mitaa Chinyami lililofanyiwa mabadiliko.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Serikali za Mitaa Chinyami yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA CHINYAMI

Makadirio ya eneo: Hekta 43,330 au Kilometa za Mraba 433.30 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la msitu wa Hifadhi Chinyami wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa linalopatikana Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 2128 (Skeli 1:50000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 1044 (Linaendelea)*




Dodoma
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*